

TAARIFA MAALUM KUHUSU HALI YA MAFUTA ZANZIBAR 20/02/2018

Kufuatia hali ya kutokua na Mafuta ya Petroli iliyojitokeza hasa katika Vituo vya Mafuta vya Kampuni ya United Petroleum (UP) na kusababisha Foleni katika Vituo vya Mafuta vya Kampuni za Zanzibar Petroleum (ZP) na GAPCO, ZURA imechukua hatua zifuatazo kukabiliana na changamoto hiyo:-

Meli ya 'United Spirit 1' inatarajiwa kupakia Mafuta ya Petroli Kesho 21/02/2018 katika Bandari ya Dar es salaam. Awali Meli hiyo ilitarajiwa kupakia Jana lakini haikufanikiwa. Aidha, Meli hiyo inatarajiwa kupakia Tani Eflu Moja (1000 Metric Tones) sawa na Lita Milioni Moja na Laki Tatu (1,300,000) za Mafuta ya Petroli.

ZURA inaendelea kusimamia zoezi la usambazaji na uuzwaji wa mafuta vituoni kwa yale yaliyopo hadi Mafuta yaliyoagizwa yatakapofika nchini na kuhakikisha yanauzwa kwa mujibu wa maelekezo ya Mamlaka. Pia ZURA inaendelea na juhudi mbali mbali ikiwemo kukagua katika Bohari na vituo vya mafuta, kuhakikisha taratibu zote zakisheria zinafatwa na hatua zaki nidhamu zitaendelea kuchukuliwa kwa wale wote watakaokwenda kinyume na taratibu hizo.

Wananchi wanaombwa kuwa wastahamilivu, wakati Mamlaka inafanya juhudi za kutosha kuhakikisha hali ya upatikanaji wa Mafuta inarejea katika hali ya kawaida na kukidhi mahitaji ya Soko. Pia ZURA inaomba ushirikiano kutoka kwa Wadau wote wa Mafuta na Wananchi katika kukabiliana na changamoto hii.

IMETOLEWA NA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)